

Unyanyasaji wa nyumbani na wa familia haukubaliki nchini Australia

Je, mwenzi wako au mwanafamilia anafanya yoyote ifuatayo?

- Anakufanya wewe au watoto wako kuogopa?
- Anapiga au kukudhuru wewe au watoto wako?
- Anatarajia ufanye mapenzi hata ikiwa hutaki?
- Anapiga kelele, kutupa vitu, au kuvunja vitu?
- Anakutukana au kukufanya ujione huna maana?
- Anakuzuia kuwa na pesa zako mwenyewe?
- Anakuzuia kwenda mahali au kuona watu?



Ikiwa umejibu 'Ndiyo' kwa swali lolote hilo hapa juu, huenda unaishi na unyanyasaji wa nyumbani na wa familia.

Una haki. Unyanyasaji wa nyumbani na wa familia ni kinyume cha sheria. Sheria hulinda kila mtu, ikiwa ni pamoja na wahamiaji wapya na wenye viza vya muda.

Usaidizi unapatikana. Zungumza na daktari au mfanyakazi wa afya. Tutakuunga mkono ikiwa unachagua kuendeleza au kuacha uhusiano wako.

Tafadhali tuombe mtafsiri wa kitaalamu bila malipo kwa usaidizi katika lugha yako.

Mwasiliani wa eneo (Local contact)

Huduma (Service):

Simu (Phone):

Ili kupata usaidizi mwingine, simu za msaada za saa 24 zinapatikana:

1800RESPECT

1800 737 732

NSW Domestic Violence Helpline

1800 65 64 63

(Simu ya Msaada wa Unyanyasaji wa Nyumbani ya NSW)

Lifeline Australia (Shirika la Lifeline ya Australia)

13 11 14

Kwa usaidizi katika lugha yako, pigia simu Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS) kwa 131 450 na uombe kupiga simu ya usaidizi.

Katika hali ya dharura au ya kuhatarisha maisha, piga simu kwa 000.